

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA ISHIRINI**

**Kikao cha Ishirini na Tano - Tarehe 9 Juni, 2015**

(Kikao Kilanza Saa Tatu Asubuhi)

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu. Atakayeuliza swali la kwanza ni Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, kwa niaba yake Mheshimiwa Laizer. Huu UKAWA mpya umeanza lini? (Kicheko)

Na. 168

**Upungufu wa Watumishi wa Sekta  
ya Afya Wilaya ya Kilwa**

**MHE. LEKULE M. LAIZER (K.n.y. MHE. MURTAZA A. MANGUNGU)** aliuliza:-

Je, ni hatua zipo za muda mfupi na mrefu zinachukuliwa na Serikali katika kukabiliana na upungufu wa watumishi wa afya Mkoani Lindi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI  
ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kuwa kumekuwa na tatizo la upungufu wa watumishi wa sekta ya afya kwa nchi nzima ikiwemo Wilaya ya Kilwa. Kwa kuzingatia ikama ya watumishi, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa inatakiwa kuwa na watumishi wa afya 1,275 waliopo ni 375, hivyo ina upungufu wa watumishi 900 wenye sifa mbalimbali. Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Ofisi ya Rais, Menejimenti Utumishi wa Umma imekuwa ikiwapanga watumishi wa afya moja kwa moja katika vituo vya kazi baada ya kuhitimu mafunzo yao.

Changamoto kubwa iliyopo ni uhaba wa watumishi wa sekta hii katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kutekeleza azma ya kuhakikisha huduma ya afya zinapatikana na kutolewa kwa wananchi kila mwaka, Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa imekuwa ikipema vibali vya ajira na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii imekuwa ikiwapangia vituo vya kazi watumishi hao. Hizi zikiwa ni hatua za Serikali za muda mfupi. Aidha, katika mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2015/2016, Halmashauri imetenga nafasi mpya za ajira kwa asilimia 17 ya watumishi waliopo kwa sasa ambao ni sawa na idadi ya watumishi takribani 74 ambao wataendelea kupunguza tatizo la ikama ya watumishi wa sekta ya afya katika Wilaya ya Kilwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua changamoto ya ikama ya watumishi wa sekta ya afya, imeingiza sekta ya afya katika Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa ambapo moja ya kipaumbele katika sekta hii ni kuhakikisha kuwa kunakuwepo na watumishi wa kutosha katika zahanati, vituo vya afya na hospitali. Kipaumbele hicho kitagusa maeneo makuu yafuatayo:-

- (i) Vibali vipyta vitatolewa kwa mwaka kuzingatia mahitaji;
- (ii) Kuimarisha ubia na sekta binafsi;
- (iii) Kugawa upya watumishi waliopo katika mkoa, halmashauri kwa kuzingatia mahitaji;
- (iv) Kuanzisha mfumo wa mikataba inayowafunga watumishi kutoa huduma kwa kipindi fulani kabla ya kuamua kuondoka au kuweka vivutio vya watumishi kwa wale wa maeneo ya pembezoni ya nchi na kuimarisha mafunzo kazini, ili watumishi wachache waliopo wamudu kazi zao.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zinazochukuliwa na Serikali ni kuongeza udahili wa wanafunzi wanaojiunga na fani ya afya ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wanafunzi kupenda masomo ya sayansi ili hatimaye kupata watumishi wa kutosha katika sekta ya afya.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Michael Lekule Laizer swali la nyongeza.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa watumishi 900 aliosema ndiyo upungufu uliopo katika wilaya hiyo, inawezekana wengi wao ni wa zahanati za vijijini ambapo ndiko kwenye upungufu mkubwa.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Je, Serikali inafanya utaratibu gani ili zahanati zilizopo huko mbali vijijini zisiwe na upungufu wa madaktari?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa kule vijijini unakuta kwamba madaktari waliopo ni wanaume tu hamna manesi. Je, Serikali haioni kwamba kuna upungufu mkubwa wa tiba kwa akinamama ikiwa ni wanaume tu ndiyo wapo katika zahanati hizo? Kwa nini uwiano usiende sambamba, ukiangalia katika hospitali zetu za vijijini wengi waliopo huko ni wanaume kutokana na mazingira magumu na kutopelekwa akinamama?

**SPIKA:** Manesi wanaume wapo lakini, Mheshimiwa Waziri wa Nchi majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na watumishi wa kutosha katika zahanati, kama nilivyotangulia kusema ni kwamba Serikali inaongeza udahili na pia tunawapeleka watumishi bila kufanya usahili, wakimaliza tu wanapangiwa vituo vya kazi. Kinachotakiwa ni halmashauri husika kuhakikisha kwamba wanapeleka matabibu pamoja na wauguzi katika zahanati ambazo amezzungumzia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la uwiano baina ya tabibu au wauguzi wanawake kwa wanaume, nadhani ni suala la kuwapanga katika eneo la halmashauri husika. Kwa sababu ukiangalia kwa kiasi kikubwa wauguzi wengi ni wanawake kushinda hata hao wanaume anaowasema. Kwa hiyo, nisingetegemea tuwe na tatizo kubwa sana kwamba wanaoonekana kule wengi ni wanaume kuliko wanawake.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, amesema moja ya mkakati ambao wanao ni kuhakikisha kwamba wanafunzi wanadahiliwa kwenye vyuo ambavyo vinachukua fani ya afya.

Mheshimiwa Spika, napenda kuiuliza Serikali, pamoja na udahili huo kwenye vyuo mbalimbali hususan vile vya afya kama Muhimbilli, Kampala International University lakini imeonyesha wazi kwamba vyuo hivi vinasajili wanafunzi ambao hawana vigezo au vyuo vyenyewe havijapata usajili kutoka kwenye Mabaraza ya Famasia, jambo ambalo limepelekea wanafunzi kumaliza vyuo hivyo lakini hawajapata ajira. Je, Serikali inasema nini kuhusiana na hali ilivyo katika chuo hicho cha *KIU*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan unataka ku-prolong jambo ambalo linafanyiwa kazi. Mheshimiwa Waziri jibu maswali ya maana tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI**

**ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa maelekezo yako. Ninachotaka kusema ni kwamba vyuo hasa vya Serikali ambavyo tunawadahili wanachuo tunahakikisha kwamba ni lazima wawe wamesoma masomo ya sayansi. Hata hivyo, chuo chochote ambacho mwanafunzi atakuwa amesoma wakati wa kuajiri tunachoangalia ni vyeti vyake na ufaulu wake. Kwa hiyo, kama mtu amesoma elimu ya kubabaisha ambayo haitambuliwi na Serikali, hatuwezi kumpangia kituo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Najua dhamira ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni kuhakikisha inasogeza huduma za afya karibu na wananchi. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, lakini katika Jimbo la Bunda kuna kituo cha afya kikubwa cha Unyari, Mgeta lakini nasikitika kwamba wananchi wanakosa huduma kutokana na kukosekana wataalamu wa afya. Kujenga vituo vya afya ni jambo lingine lakini kuna umuhimu wa kuhakikisha kuna nyumba za watumishi. Mfano, kituo cha afya cha Unyari kimezungukwa na Mbuga ya Serengeti, ni vigumu kwa mazingira ya nyumba za wananchi watu wale wakarisk kukaa pale na kupata matatizo ya kusumbuliwa na wanyama. Ni lini Serikali itahakikisha inaweka miundombinu bora ili wananchi wa Bunda, Unyari na Mgeta wapate hiyo huduma ya afya inayostahiki?

**SPIKA:** Kweli umekabidhiwa. Mheshimiwa Waziri wa Nchi. (Kicheko)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI**

**ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la miundombinu, kwanza, ielewewe Serikali ni pamoja na Serikali Kuu, Serikali za Mitaa lakini ni pamoja na sisi. Tunaposema suala la mipango, sisi TAMISEMI au Wizarani hatupangi mipango ya halmashauri, halmashauri zenyewe ndizo zinazoanzisha mipango inakuja huku kwetu. Kwa hiyo, kama sisi TAMISEMI au Wizara yoyote hatuwezi kuona na kujua yaliyopo katika maeneo yetu. Kwa hiyo, ni suala letu sisi, wakiwemo Madiwani, Wabunge na wananchi walioko katika maeneo yale, kuhakikisha wakati tunapoandaa mipango basi ilenge vipaumbele ambavyo ndio matatizo halisi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wenzangu, tujikite kule inapotokea mipango badala ya kuja huku, huku hatupangi mipango, huku tunapitisha tu yale ambayo tumeyapanga kule tulikotoka.

**SPIKA:** Tumetumia dakika kumi na tatu kwa swali moja. Sasa twende Ofisi ya Rais, Utawala Bora, Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis.

Na. 169

**Ukiukwaji wa Maadili kwa Viongozi wa Umma**

**MHE. FAKHARIA S. KHAMIS** aliuliza:-

Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeweka mifumo mbalimbali ya kusimamia maadili ya viongozi ili kuhakikisha kwamba majukumu ya umma yanatekelezwa kwa namna ambayo inajenga na kulinda imani ya wananchi juu ya Serikali yao; pamoja na mienendo ya viongozi katika utekelezaji wa majukumu ya umma kwa misingi ya uwazi, uwajibikaji, uaminifu, haki, huruma na umaskini kwa kujizua na tamaa:-

Je, ni viongozi wangapi ambao tayari wamefikishwa Tume ya Maadili na kuhukumiwa kutokana na makosa ya ukiukwaji wa maadili?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka wa fedha 2010/2011 hadi 2014/2015, jumla ya viongozi 73 walifikishwa mbele ya Baraza la Maadili kwa sababu mbalimbali zikiwemo kushindwa kutoa tamko la rasilimali na madeni, matumizi mabaya ya madaraka, kutoa tamko la uongo, kutotamka maslahi ya mkataba na Serikali na kutotamka zawadi. Kati ya malalamiko 73 yaliyofikishwa mbele ya Baraza, viongozi kumi na nane hawakupatikana na hatia, 29 walipatikana na hatia na kupewa adhabu mbalimbali kama ifuatavyo:-

- (i) Viongozi 14 walipewa onyo;
- (ii) Viongozi 10 walipewa onyo kali;
- (iii) Viongozi wanne (4) walipewa onyo na tahadhari; na
- (iv) Kiongozi mmoja alitozwa faini.

Mheshimiwa Spika, malalamiko 26 yaliyobaki yako kwenye hatua mbalimbali, ikiwemo 17 ambayo yameahirishwa kusikilizwa na Baraza, malamiko matatu (3) yanashubiri uamuvi wa Mahakama Kuu kufuatia walalamikiwa kuomba kupinga uamuvi mdogo wa Baraza wa kuendelea kuchunguzwa.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Aidha, Baraza limekubali lalamiko moja liendelee katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu. Lamako matano (5) yamekamilika na taarifa yake imewasilishwa kwenye mamlaka husika kwa utekelezaji wa mapendekezo ya Baraza la Maadili.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Fakharia swali la nyongeza.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa ufanuzi wake, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kiongozi anapopelekwa kwenye Sekretarieti ya Maadili, umma wa Watanzania wote wanapewa taarifa. Je, ni kwa nini hatua zinapochukuliwa kwa kiongozi yule umma wa Watanzania hautaarifiwi ili na wao wakafahamu kama kiongozi yule kaingia kwenye hatia au hajaingia? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ikiwa kuna sheria ambayo ndiyo kikwazo inayokataza kuwapa Watanzania taarifa ya hatua iliyochukuliwa kwa kiongozi yule, je, hampo tayari sheria hiyo kuileta tena Bungeni ikarekebishwa ili Watanzania wakawa wanajua kiongozi wao aliyepelekwa kwenye Sekretarieti ya Maadili amechukuliwa hatua fulani au hakuwa na hatia?

Mheshimiwa Spika, naomba nipate majibu ya hayo maswali mawili. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, kwanza anataka kujua kwa nini hatutangaziwi kesi imeishaje au adhabu ili wananchi wakajua kama yule mtu amepatwa na hatia au hapana. Sheria tuliyonayo sasa inaruhusu mtu yeyote anayetaka kwenda kusikiliza Baraza linavyoendeshwa. Kuhusu adhabu inayotolewa, utaona kwamba katika adhabu zilizotamkwa mle, mtoaji adhabu mara nyingi ni mamlaka husika. Baraza hili likimaliza uchunguzi linamshauri mwenye mamlaka husika. Chukulia kwa mfano kama ni Mkurugenzi, itapelekwa kwa Waziri Mkuu, kama ni Mkuu wa Wilaya, itapelekwa kwa Rais. Ikishakuwa imepelekwa kule, anayetoa adhabu kule yeye ndiye ana fursa ya kutangaza kama Mkuu wa Wilaya kamfukuza, itatangazwa. Kwa hiyo, Baraza linakaribisha watu kwenda kusikiliza lakini baada ya pale linapeleka mapendekezo kwa mamlaka husika, huko ndipo kunachukuliwa hatua.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ameeleza kwamba kuna tatizo/kikwazo chochote kwenye sheria kwa nini tusifanye mabadiliko. Nataka kusema kwamba katika Katiba Inayopendekezwa endapo itapita kwa wananchi, marekebisho makubwa yamefanyika lakini hata kabla hiyo Katiba inayopendekezwa haijafanyiwa kazi, tumeleta hapa Bungeni, tunasubiri tu kupangiwa ratiba, sheria ya marekebisho ya sheria hii ili tubadilishe baadhi ya vifungu. Kwa mfano, sheria sasa inasema ukipata zawadi ya Sh.50,000, uje umueleza Afisa Mhasibu, tunapendekeza kwamba imepitwa na wakati na vifungu vingine vingine. Kwa hiyo, wakati tunasubiri kwenda kwenye Katiba mpya, tutaleta hapa Bungeni marekebisho ya sheria kama Mheshimiwa Mbunge anavyoshauri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Kahigi.

**MHE. PROF. KULIKOYELA K. KAHIGI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hili eneo la utawala bora, kwa kweli lina matatizo makubwa sana kwa sababu Serikali haijachukua hatua thabit na ndiyo yanayosababisha rushwa na ujisadi katika maeneo mengi. Kwa kuwa, Serikali ina utaratibu wa Matokeo Makubwa Sasa, ina mikakati gani ili iondoe haya matatizo yote ambayo yanalikabili eneo hili la utawala bora?

**SPIKA:** Yaani Matokeo Makubwa Sasa iende na huko, Waziri wa Nchi jibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, kwanza siyo kweli kwamba Serikali haijachukua hatua madhubuti katika suala la kupambana na rushwa.

Ili upambane na rushwa ni lazima pawepo na *political will* (utashi wa kisiasa). Serikali ya CCM ina utashi wa kisiasa, imeweka katika llani ya Uchaguzi, imeanzisha chombo cha TAKUKURU, imepanua na imeimarisha utendaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu BRN, mimi ninayezungumza hapa ni Mwenyekiti wa Kamati ya BRN ya kuondoa vikwazo katika biashara na mahali popote kwenye viashiria vya rushwa, tunafanya kazi nzuri. Kwa mfano, kule bandarini kila mwezi walikuwa wanaiba makontena 30, tangu tumeanza Kamati hii ya BRN hakuna kontena hata moja linaloibowi kule bandarini. Pili, kulikuwa na vituo vingi sana kutoka Dar es Salaam kwenda Burundi, Congo mtu anasimamishwa mara karibu 15, tumevipunguza vile sasa imebaki karibu vitano tu. Kwa hiyo, kazi inafanyika na wananchi wanaona. (Makofij)

**SPIKA:** Maswali yanakuwa mrefu, majibu mrefu, swali moja linachukua dakika 13, haiwezekani. Sasa tunaenda kwa speed zaidi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba atauliza swali hilo, kwa niaba yake Mheshimiwa Vick Kamata, sijakusikia siku nydingi.

Na. 170

**Kulipa Madeni ya Walimu**

**MHE. VICK P. KAMATA (K.n.y. MHE. LOLESLIA J. BUKWIMBA)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa madeni ya Walimu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, Mbunge wa Busanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, madai ya walimu yalihu malimbikizo ya mishahara (PE) na yale yanayotokana na matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2014/2015. Madai ya malimbikizo ya mishahara ya walimu yaliyowasilishwa Serikali yalifikia Sh.57,225,827,261.24. Madai haya yalihu walimu 78,112.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kati ya mwezi Julai 2014 hadi Aprili, 2015, walimu 31,706 walilipwa Sh.24,970,752.61 kama malimbikizo yao ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, madai ya malimbikizo ya mishahara ya walimu 27,451 yenye kiwango cha Sh.13,620,031,300 yalifutwa kwa sababu hayakuthibitika kuwa halali kulingana na mfumo wa malipo ya mishahara. Aidha, madai ya malimbikizo ya mishahara ya walimu 3,356 yenye kiwango cha Sh.3,726,562,168.01 yaliyowasilishwa kwa kutumia fomu maalum za madai yamerudishwa kwa mamlaka ya ajira za walimu hao ili wayafanyie marekebisho stahiki na kuyawasilisha tena ili yaweze kulipwa.

Mheshimiwa Spika, madai ya malimbikizo ya mishahara ya walimu 150 yenye kiwango cha Sh.282,971,830.96 tayari yameingizwa kwenye mfumo wa malipo ya mishahara kwa ajili ya kulipwa kupitia orodha ya malipo ya mishahara mwezi Juni, 2015.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, madai yasiyo ya mishahara yaliyowasilishwa yalikuwa Sh.19,631,843,225.92. Baada ya kuhakikiwa iligunduliwa kuwa madai halali yalikuwa Sh.5,665,772,117.93 ambapo kati ya fedha hizo kiasi cha Sh.5,378,829,715 .93 zimelipwa kwa walimu walio chini ya TAMISEMI na Sh.286,942,402 zimelipwa kwa walimu wakufunzi walio chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu.

Mheshimiwa Spika, madai mengine ya Sh.10,591,891,368.99 kutoka TAMISEMI na Sh.1,574,177,396 kutoka Wizara ya Elimu yalikataliwa baada ya kubainika kuwa baadhi tayari yalikwishalipwa na mengine yalikuwa na vielelezo vya makosa.

Mheshimiwa Spika, naomba kupitia Bunge lako Tukufu kutoa wito kwa Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambao wamerudishiwa fomu ambazo zilikuwa na makosa ili waweze kuzirekebisha wazishughulikie haraka iwezekanavyo ili madai haya yaweze kulipwa mwezi Julai 2015.

**SPIKA:** Kweli lilikuwa swali refu, Mheshimiwa Vick Kamata swali la nyongeza!

**MHE. VICK P. KAMATA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Mkoani Geita mpaka sasa kuna zaidi ya walimu 1000 wamesharipoti lakini hakuna pesa yoyote ambayo imelipwa na wanaishi katika mazingira magumu sana. Ni nini tamko la Serikali juu ya suala hilo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita wamekuwa wakipewa pesa yao ya likizo nusunusu kitu ambacho kinapelekea washindwe kwenda likizo. Nini tamko la Serikali juu ya suala hilo pia? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante kwa kuuliza kwa kifupi. Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, nadhani swali hili namjibu na Mheshimiwa Selasini, nimeona akipiga makofi sana likiendana na swali lake ambalo aliliuliza jana.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza tumepeleka walimu 28,007 na kati ya hao waliokuwa wameripoti ni 26,046 sawa na asilimia 93. Kati ya hao, walimu 23,180 tayari wamelipwa mishahara ya mwezi Mei ambao ni sawa na asilimia 89. Walimu ambao hawajalipwa mishahara kati ya hao walioripoti ni 2,866 tu. Sababu za kutokulipwa mishahara baadhi yao ni kwamba wameenda bila vyeti halisi na baadhi yao walijaza fomu za ajira vibaya.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mheshimiwa Selasini, kati ya walimu 432 ambao tumempangia walikuwa wameripoti 348 na kati ya hao walimu 275 wamepata mshahara wa mwezi Mei. Katika posho za kujikimu, walimu wote walioripoti Rombo wamelipwa posho ya kujikimu ya siku nne wanadai siku tatu ambazo tunasubiri kutoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, nikirudi kwa Mheshimiwa Vick Kamata ni kwamba tulizielekeza halmashauri zote kwa sababu sasa hivi katika halmashauri pesa zipo nyingi na hazijatumika, tumewaaagiza watumie pesa zile wakati tukisubiri pesa kutoka Hazina ambazo tunazitegemea kuzipata wakati wowote.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa David Ernest Silinde atauliza swali hilo.

Na. 171

#### **Hitaji la Mawasiliano ya Simu Eneo la Chitete-Momba**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Eneo la Chitete ambapo ndiyo Makao Makuu ya Wilaya Mpya ya Momba linakabiliwa na ukosefu wa mawasiliano ya simu:-

Je, ni lini eneo hilo litapatiwa mawasiliano ya uhakika ya simu?

**NAIBU WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kata ya Chitete katika Wilaya ya Momba, Mkoani Mbeya imejumuishwa katika Mradi wa Mawasiliano Vijiji Awamu ya Kwanza (Phase IA) unaosimamiwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ambapo kampuni ya mawasiliano ya Vodacom ilishinda zabuni ya kupeleka mawasiliano hayo. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 30, 2015.

**SPIKA:** Mheshimiwa Silinde swali la nyongeza.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Najua swali langu hili niliuliza zamani, moja niseme tu kwamba nawashukuru Wizara kwa kutekeleza, mimi mwenyewe nimeshuhudia hiyo kitu na maeneo yote niliyoomba wamepeleka minara ya simu, kwa hilo nawashukuru. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nina swali dogo tu, kuna maeneo kwa mfano Kata za Kapele, Miyunga na Nzoka ambako mawasiliano bado ni shida kidogo. Ningombwa *commitment* ya Serikali kuhusiana na maeneo haya. Hilo ndiyo swali langu la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swali dogo la pili ni kwamba kule vijiji watu wanaotumia simu hizi, wanapokuwa wanaomba vifurushi (*bundle*) wanakatwa na data wakati simu zao nydingi hazina uwezo wa kutumia *internet*. Sasa nataka kauli ya Serikali kwa nini wanakata fedha za wananchi za data wakati data hizo hawatumii, kwa nini wasiweze kutenganisha kwenye hilo?

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa niaba.

**NAIBU WAZIRI WA AFRIKA MASHARIKI (K.n.y. WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru kwa kuishukuru Serikali na ndiyo jitihada ambayo inafanywa lakini ni lazima nitoe taarifa tu kwamba katika vijiji ambavyo amevitaja kuna mipango miwili sasa hivi inaendelea. Mpango wa kwanza ni ule ambao Mheshimiwa Waziri aliwaombeni Wabunge kuonyesha ni sehemu gani ambazo zina mawasiliano kidogo ambao unasimamiwa na Mfuko wa Mawasiliano wa Pamoja. Mikakati imeanza tangu Desemba mwaka jana lakini taratibu kidogo zilikawia kutokana na masuala ya manunuvi. Mpango mwengine, hivi sasa kuna kampuni ya Viettel ambapo mkipita sehemu tofauti mtaona wamechimba, hawa wamepewa mradi wa kufungua mawasiliano katika vijiji 4000 katika phase tatu.

Mheshimiwa Spika, ukichukua hii mipango miwili yaani huu wa Viettel pamoja na ule mradi wa mawasiliano lakini pia kuna mradi mmoja Mheshimiwa Keissy alikuwa anauzungumza sana wa kule mpakani, pamoja na pesa za Serikali kutoka *Consolidated Fund* zitashughulikia masuala hayo. Kwa hiyo, kuhusu jambo hilo msiwe na wasiwasi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la data, hili kidogo ni mtihani, niseme tu nitashindwa kujibu kwa sababu taratibu zile ni za kisayansi ndani ya zile simu zenyewe. Maana hata mimi mwenyewe inatokea wakati mwengine nikijisahau naona zimekwenda tu. Kwa hiyo, nashindwa kulijibu labda nilichukue baadaye tukutane mimi na wewe tulifanyie kazi. Ahsante sana. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa AG majibu ya nyongeza.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nalishukuru Bunge lako Tukufu kwamba kwenye Mkutano wa 19 Bunge hili lilipitisha sheria mbili, moja inaitwa *The Electronic Transaction Act* na nyingine inaitwa *The Cyber Crime Act*. Sheria hizi zinakusudia ku-regulate matumizi ya electronic. Swali la mwisho alilosema Mheshimiwa Silinde linadhibitiwa na hizo sheria na hasa ya *Cyber Crime*, kwa kweli tatizo hili ni kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, sheria hizi baada ya kupitishwa zimeshasainiwa na Mheshimiwa Rais, sasa tunaandaa Kanuni zake ili zianze kutumika. Nia yangu ni kwamba matumizi ya sheria hizi yaanze mapema ili kudhibiti vitendo hivyo vya uhalifu. Kuna hujuma nyingi sana mtandaoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niwasihi Waheshimiwa Wabunge waendelee kuipa ushirikiano Serikali inapotekeleza jukumu lake la msingi la kusimamia utekelezaji wa sheria nchini.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Tunaenda Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Rajab Mbarouk atauliza swali.

Na. 172

**Magonjwa Yanayoenezwa kwa  
Matumizi ya Chakula Kisichokuwa salama**

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED** aliuliza:-

Shirika la Afya Duniani (WHO) linathibitisha kwamba magonjwa zaidi ya 200 duniani yanaenezwa kwa njia ya matumizi ya chakula kisichokuwa salama; na inakadirisha  $\frac{1}{3}$  ya wakazi wa nchi zinazoendelea wanakabiliwa na magonjwa yanayotokana na chakula kila mwaka:-

(a) Je, hali halisi ikoje kwa Tanzania?

(b) Je, hadi sasa *TFDA* imeshafanya kaguzi ngapi ili kugundua viwanda vya aina gani na vingapi ambavyo ni hatarishi vya usindikaji wa vyakula?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohammed, Mbunge wa Jimbo la Ole, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, chakula kisichokuwa salama ni kile ambacho kimechafuliwa na kemikali, vimelea vya magonjwa na vyanzo vingine katika kiwango ambacho kinaweza kuleta athari za kiafya kwa mlaji. Vichafuzi hivi vinaweza kuleta athari za kiafya katika muda mfupi (*acute*) au baada ya muda mrefu (*chronic*) kama vile magonjwa ya saratani.

Kwa kuzingatia kuwa afya ya walaji wa chakula inaweza kuhatarishwa kutokana na kula chakula kisichokuwa salama, mwaka 2008, TFDA ilianzisha mpango wa ufuatiliaji wa magonjwa yanayotokana na chakula na ukusanyaji wa takwimu zake hapa nchini. Mpango huu ulianza kutekelezwa kwa majaribio katika Mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara kwa kutumia mwongozo wa uchunguzi na ufuatiliaji wa magonjwa yanayotokana na chakula kisichokuwa salama. Matokeo ya takwimu zilizokusanywa mwaka 2009 hadi 2012 katika mikoa hii yalionesha kuwa jumla ya watu wapatao 1,034 waliugua magonjwa mbalimbali yaliyosababishwa na matumizi ya chakula kisichokuwa salama ambapo mwaka 2009 walikuwa 307, mwaka 2010 walikuwa 271 na mwaka 2011 walikuwa 243 na mwaka 2012 ni 213.

Aidha, jumla ya watu 23 waliripotiwa kupoteza maisha katika kipindi hicho. Magonjwa yaliyoripotiwa ni pamoja kipundupindu, kuhara damu, minyoo, *brucellosis*, amiba, *shigellosis*, homa ya matumbo, madhara yanayotokana na kula uyoga wenye sumu na kimeta.

Baada ya kutekelezwa kwa ufanisi katika eneo la majaribio, mpango huu unasambazwa nchi nzima na kuzingatia upatikanaji wa rasilimali fedha. Katika kipindi cha mwaka 2013/2015, mpango umesambazwa katika Mikoa ya Kigoma, Katavi, Rukwa na Tabora.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, TFDA imekuwa ikifanya ukaguzi ili kuhakikisha kuwa vyakula kwenye soko ni salama kwa matumizi ya binadamu. Kaguzi hizi hufanyika katika hatua za usindikaji, uhifadhi na usafirishaji wa chakula. Kwa upande wa viwanda vya chakula mpaka mwezi Februari 2015, jumla ya viwanda 868 vimesajiliwa baada ya kukidhi matakwa ya kisheria.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Rajab Mbarouk maswali ya nyongeza.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, TFDA chini ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya mwaka 2003, ina jukumu kwa kweli la kusimamia ubora wa madawa, vipodozi, chakula na vifaa tiba. Hapa mimi nimezungumzia suala la chakula kisichokuwa salama.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya Naibu Waziri alichoweza kunieleza kuhusiana na swali langu la kwanza la hali halisi ilivyo, amezungumzia maradhi yale ambayo yanatokea hususan wakati wa milipuko. Labda pengine Waziri atakapokuja anieleze sasa kuhusiana na yale magonjwa ni *chronic* ambayo yanababishwa hasa na usalama au utumiaji huu wa chakula ambacho hakipo salama.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna viwanda ambavyo tunaviita viwanda hatarishi ambavyo husindika vyakula. Juzi tu hapa wakati tunachangia katika Wizara ile, tulizungumzia hata kiwanda ambacho kinasindika nyama ya punda na nashukuru Waziri aliweza kulijibu vizuri.

Sasa nataka kujua, je, hadi sasa ni viwanda vingapi ambavyo vinasindika vyakula hatarishi au viwanda hatarishi ambavyo vinasindika vyakula ambapo TFDA tayari imeshavichukulia hatua za kinidhamu kwa kukosa ubora wa chakula hicho?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, anapenda kufahamu ni magonjwa yapi ya muda mrefu (*chronic*) ambayo yanatokana na ulaji wa vyakula ambavyo siyo salama. Suala hili lina upana wake lakini kwa sehemu kubwa kama chakula kilikuwa na kemikali ambayo inaweza kusababisha saratani, saratani inaweza ikajitokeza kama tatizo la muda mrefu kutokana na ulaji wa vyakula vyenye kemikali hizo. Magonjwa mengine ni kutokana na ulaji wa chakula ambacho kina visababishi vya magonjwa kwa mfano ya njia ya hewa, kama vumbivumbi limetifuka kutokana na asbestos, inaweza ikaingia kwenye chakula ambapo mtu anaweza akavuta ile hewa baadaye akapata tatizo la ugonjwa wa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, swali lingine kwamba ni viwanda vingapi ambavyo TFDA wameweza kuvibaini, kama nilivyojibu katika swali la msingi, jumla ya viwanda vilivyopitiwa katika kipindi cha mwaka jana hadi mwaka huu ni 868. Katika maeneo hayo, viwanda vile ambavyo labda vimeonekana kuwa na kemikali, tutaleta orodha ile na kuiwasilisha hapa Bungeni kwa sababu ni swali linalojitegemea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari.

**MHE. DKT. MAUA A. DAFTARI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mimi nataka nitolewe wasiwasi kidogo na Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa wananchi wengi sasa hivi wamehamasika kusindika mafuta na ukitoka Dar-es-Salaam mpaka Morogoro unakuta magaloni mengi ya mafuta lakini ya rangi tofauti. Je, mafuta haya yamepimwa na usalama wake kwa sisi watumiaji ukoje? (Makofii)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Katika maeneo ya kuhifadhi mafuta yakiwemo ya alizeti, ni kweli yanaweza kuwekwa katika maeneo ya wazi na kutokana na hali ya mwanga wa jua hususan miale ya *ultraviolet* yanaweza yakawa yametoka katika kiwango chake cha ubora. Ndiyo sababu tunafanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ili kusudi mafuta yale yaweze kuhifadhiwa vizuri. Hata hivyo, katika soko, mara nyingi mafuta yale hayawezi kukaa pale zaidi ya mwezi mmoja. Ufuatiliaji ambao umefanyika kama yamekaa kwenye jua zaidi ya mwezi mmoja, yanaweza yakabadilika na kuwa katika kiwango ambacho hakifai.

Mheshimiwa Spika, natoa maelekezo kwa nchi nzima na kanda zetu sita ambazo tunazo, kanda moja mwakani tutafungua kule Kusini, usimamizi na ufuatiliaji ufanyike kwa ukaribu kama ilivyo kwa kila robo ya mwaka kufanya ukaguzi katika maeneo yote yale ambayo kuna vyakula na vitu vingine ikiwemo dawa na vipodozi ili kusudi kuhakikisha kwamba Watanzania wanakula vyakula ambavyo vina ubora.

**SPIKA:** Ahsante. Tuendelee na Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya.

Na. 173

### **Matumizi ya Vipodozi**

**MHE. MUHAMMAD IIBRAHIM SANYA** aliuliza:-

Akinamama wengi hapa nchini hutumia vipodozi ambavyo havina viwango vinavyofaa kwa matumizi ya binadamu; pamoja na jitihada za Serikali kuzuia bidhaa hizo lakini bado zinaingizwa nchini:-

Je, ni lini Serikali itakuwa makini katika bidhaa hizo zisiendelee kuingizwa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Muhammad Ibrahim Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuitia Mamlaka ya Chakula, Dawa na Vipodozi (*TFDA*) imeweka utaratibu wa kudhibiti uingizaji na utoaji nje ya nchi wa vipodozi pamoja na bidhaa nyine inazodhibiti (*import and export control*).

Mheshimiwa Spika, bidhaa za vipodozi pia husajiliwa na *TFDA* kabla ya kuruhusiwa kutumika nchini. Jitihada mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa kudhibiti uingizaji wa vipodozi nchini ikiwa ni pamoja na kuhakikisha vipodozi vilivyosajiliwa tu ndiyo vinaingia na kutumika hapa nchini; kusajili maeneo yanayojihuisha na biashara ya vipodozi na kuchukua sampuli kwenye soko na kuzipima kwenye maabara ya *TFDA* ili kuhakiki ubora wake.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa *TFDA* imesajili jumla ya vipodozi vipatavyo 2,527 ambavyo hivyo vinaruhusiwa kuingizwa na kutumika nchini. Vilevile kwa mwaka wa fedha 2014/2015 mabasi ya abiria matatu yalikamatwa mkoani Mbeya na Dar-es-Salaam yakiwa yamebeba vipodozi ambavyo vimesajiliwa kutoka nchi jirani na wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria. Katika mwaka 2014/2015, jumla ya tani zipatazo 16.61 za vipodozi vilivyopigwa marufuku vyenye thamani ya shilingi za Kitanzania milioni 44.2 zimeteketeza na *TFDA*.

Mheshimiwa Spika, elimu pia imekuwa ikitolewa juu ya matumizi sahihi ya vipodozi. Mfano mwaka 2014/2015, shule 16 zilitembelewa na elimu kutolewa juu ya matumizi ya vipodozi. *TFDA* pia ilishirikisha taasisi mbalimbali binafsi mfano Envirocare katika kuhamasisha jamii juu ya matumizi ya vipodozi.

Mheshimiwa Spika, hatua zimechukuliwa pia kufanya mawasiliano na nchi jirani, mfano Zambia kuitia mpaka wa Tunduma, ili kuzuia vipodozi visiingie nchini kutoka huko. Kupitia mpango wa kuwianisha Mfumo wa Udhibiti wa Dawa katika nchi hizi za Jumuia ya Afrika Mashariki Kusini mwa Afrika (*East African Community and SADC Medicines Regulatory Harmonization Programmes*), tunatarajia kuweka mkakati wa kushirikiana kudhibiti bidhaa mpakani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sanya, maswali ya nyongeza!

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa inaonekana kwamba matumizi ya vipodozi yanaendelea kukua mwaka hadi mwaka nchini kwetu na kwa kuwa athari zake zimekuwa ni kubwa na udhibiti wa kuingiza bidhaa hizo ambazo hazikubaliki umekuwa ni mdogo. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba wakati umefika yeye kuzungumza na Waziri wa Elimu ili katika somo la sayansi kuanzia primary, ikaingizwa athari za matumizi ya vipodozi kuanzialili watoto wetu wote wa kike na wa kiume waelewe na kuoneshwa picha zinazoathiri watu wanaotumia madawa hayo? (Makofij)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa vile hili ni suala la kibiashara na kupoteza kama hizo shilingi milioni 44 kwa wafanyabiashara ambao wameingiza bidhaa ambayo iko chini ya kiwango ni athari kubwa kiuchumi kwa wafanyabiashara wetu. Kuna makampuni makubwa duniani ambayo yanatengeneza bidhaa hizi zenye viwango kama vile Revlon, Estee Lauder, Clarins, MAC, kwa nini Serikali isizungumze na kampuni hizi, wakaja wakafungua viwanda vidogovidogo vya kutengenezea vipodozi na kuzuia kabisa vipodozi kutoka nchi za nje ili uchumi ukakua na wanawake wetu nchini wakatumia vipodozi vyenye viwango ambavyo vinakubalika na athari yake inakuwa ni ndogo?

**SPIKA:** Haya, wewe unajua je? Mheshimiwa Naibu Waziri. (Kicheko)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa kazi nzuri anayoifanya Mheshimiwa Sanya, suala hili amelifuatilia kwa muda mrefu na tunaomba uendelee na moyo huo lakini kama unaona kule kuna kubanana kidogo rudi nyumbani Chama cha Mapinduzi. (Kicheko/Makofij)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya kwanza ya swali lake kuhusu kufundisha mashulenii, programu hiyo tumeshaianza na tutaendelea kufundisha hususan katika umri ule wa mabinti hasa ambao wanatumia vipodozi hivi japo wamo wanaume au wavulana wengine nao huwa wanatumia vipodozi. Tutaendelea kushirikiana kwa mawazo mazuri kama ambavyo tumeshirikiana tangu 2009 kufundisha katika mashule hususan shule za msingi, darasa la sita na la saba na shule zote za sekondari na vyuoni athari ambazo zinawapata watumiaji.

Mheshimiwa Spika, nashukuru katika swali ambalo liliulizwa, namba 166, nilitoa maelezo kwamba matumizi ya hivi vipodozi vinakuwa na viambata ambavyo vinakuwa na madini tembo (*heavy metals*) ikiwemo mercury (*zebaki*). Madini haya yana athari kubwa kwa hiyo tunatoa tahadhari kwa watumiaji wa vipodozi hivi ikiwemo mikorogo, haina viwango kuna viambata ambavyo vina sumu.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili kwamba hawa wawekezaji wa vipodozi ambao Mheshimiwa Sanya amewataja kutoka nje ya nchi, kupitia free labour market, suala la biashara huria wawekezaji hao tunawakaribisha waje, kama Mheshimiwa Sanya anao, awalete wafuate utaratibu wa uwekezaji nchini, wanakaribishwa sana, hakuna tatizo. Hii itasaidia sana kupunguza gharama kama alivyoshauri, hiyo ni kweli.

**SPIKA:** Lazima nimpe nafasi Mheshimiwa Joyce Mukya maana sijawahi kumsikia. (Makofi)

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza vipodozi hivi vinatumwa na wanaume pia na siyo wanawake tu kama ilivyoulizwa kwenye swali la Mheshimiwa Sanya. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vipodozi hivi vingi vinaingizwa kupitia njia za panya kupitia mipakani. Shirika la TBS lina wafanyakazi 230 tu ukilinganisha na KBS ya Kenya ambayo ina wafanyakazi 1,000 na Tanzania ina mipaka mingi sana ya kuingiza vipodozi hivi ikiwemo na bidhaa zingine, lakini nchi ya Kenya ina mipaka michache kuliko Tanzania. Je, Serikali hii haioni umuhimu wa kuongeza wafanyakazi katika Shirika la TBS? (Makofi/Vigelegele)

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli suala zima la upungufu wa watumishi nchini ni pana na wenzetu wa TBS ambao tunashirikiana nao vizuri sana katika masuala ya udhibiti na ubora wa viwango nchini, suala hili linaikumba hata Wizara ya Afya kupitia TFDA. Kwa hiyo, kazi hii itakwenda kwa pamoja kama ulivyo mpango wa Serikali wa kuendelea kuongeza watumishi Wizara kwa Wizara, Idara kwa Idara, mwaka kwa mwaka. Kwa hiyo, suala hili tutashirikiana vizuri na Idara zingine, ikiwemo Wizara ya Biashara na Viwanda ambako ndiko wenzetu wa TBS wapo pamoja na kwamba hata sisi Wizara ya Afya kupitia TFDA hadi sasa tunaao watumishi wapatao 230, ukiangalia wakati tunaanza TFDA kwa Sheria Namba 01 ya mwaka 2003 tulikuwa na watumishi 52 tu. Kwa hiyo, upungufu huu ni mkubwa katika Kanda hizi ambazo tunaendelea kupanua lakini mpango wa kuongeza watumishi ni endelelu, kama Serikali tutaendelea kuongeza.

**SPIKA:** Ahsante. Naomba tuendelee na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa atauliza swali hilo.

**Ujenzi wa Barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara Mbeya – Chunya – Makongorosi kwa kipande kilichobaki?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Jimbo la Lupa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi yenyewe urefu wa kilometra 118 ni sehemu ya barabara kuu ya Mbeya – Chunya – Makongorosi – Rungwa – Itigi – Mkiwa kilometra 528 inayounganisha Mikoa ya Mbeya na Singida. Sehemu ya barabara ya Mbeya – Makongorosi ilifanyiwa usanifu kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami ambapo utekelezaji wa kazi ya ujenzi umegawanywa katika sehemu tatu ambazo ni Mbeya – Lwanjilo kilometra 36, Lwanjilo – Chunya kilometra 36 na Chunya – Makongorosi kilometra 43. Ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Chunya – Makongorosi kilometra 43, unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2015/2016.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwambalaswa swalii la nyongeza.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwanza kabisa, napenda kuishukuru sana Serikali kwa kuanza kujenga barabara hii ya Mbeya – Chunya – Makongorosi.

Pia, napenda nichukue nafasi hii kuwaambia wananchi wa maeneo ambayo inapita barabara hii, pamoja na kwamba barabara imeleta maendeleo lakini vifo vimeongezeka mno. Kwa hiyo, wananchi wawe makini sana wanapotumia barabara hii hasahasa wanaoendesha bodaboda.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa sehemu ya Mbeya – Lwanjilo mkandarasi ni tofauti na Lwanjilo – Chunya na imeonesha kwamba mkandarasi aliyejenga kutoka Lwanjilo - Chunya amekwenda kwa kasi nzuri na ubora mzuri. Je, ni mkandarasi huyohuyo ambaye ataendeleza kutoka Chunya - Makongorosi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa barabara hii ya Mbeya – Chunya – Makongorosi - Mkiwa inaunganisha mikoa ya Mbeya na Singida. Je, ujenzi wa barabara hiyo kwa kuanzia Makongorosi - Mkiwa ambapo ni kama kilometra 413 utaanza lini?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza barabara ya kuanzia Mbeya – Lwanjilo na Lwanjilo – Chunya pamoja na kwamba ni mikataba miwili lakini mkandarasi ni yuleyule. Kwa hiyo, ana mikataba miwili, ameanza kumaliza kipande cha Lwanjilo – Chunya na sasa anaendelea kukamilisha kipande cha Mbeya – Lwanjilo.

Mheshimiwa Spika, swali kama ni huyo ataendelea na kile kipande kingine, siwezi kutoa majibu kwa sababu kazi hiyo tenda yake haijatangazwa, anaweza akaomba au asiombe. Taratibu za zabuni zitafuatwa tuweze kupata mkandarasi ambaye anaweza akafanya kazi ile.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu kuanzia pale Makongorosi - Mkiwa, je, kazi ile itaanza lini? Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, tumeshakamilisha usanifu Serikali inatafuta fedha. Miradi yote hiyo inajengwa kwa kutumia fedha za ndani, fedha za Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete. Kwa hiyo, tutaangalia upatikanaji wa fedha na ndiyo tutapanga lini tuweze kuanza kipande hicho kingine.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo swali lingine!

Na. 175

#### **Ahadi ya Ujenzi wa Barabara ya Singida Mjini hadi Ilongero kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Mheshimiwa Rais aliahidi kujenga barabara kutoka Singida Mjini hadi Ilongero kwa kiwango cha lami; na kwenye mpango wa utekelezaji wa miaka mitano ujenzi huu ulikuwa ufanyike katika mwaka wa fedha 2014/2015 lakini hadi sasa hakuna dalili ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

**NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, naomba nijibu swalii la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Singida – Ilongero kilometra 21.64 ni sehemu ya barabara ya Mkoa wa Singida kutoka Singida – Ilongero – Mtinko – Nkungi – Kidarafa – Haydom yenye urefu wa kilometra 96.36 inayohudumiwa na Wizara ya Ujenzi kuitia Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Singida na Manyara.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais, Serikali imeshaanza kujenga kwa kiwango cha lami sehemu ya barabara ya Singida – Ilongero kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, jumla ya kilometra tatu zilijengwa kwa kiwango cha lami kuanzia Singida Mjini kuelekea Ilongero kwa gharama ya shilingi milioni 900. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, jumla ya shilingi milioni 700 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kilometra mbili katika barabara hii na hivi sasa mkandarasi anaendelea na kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara hii kwa awamu kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Chilolo maswali ya nyongeza.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa barabara hii Mheshimiwa Naibu Waziri amekiri kwamba ina urefu wa kilometra 21.5 na kwa kuwa bajeti ya 2013/2014 walitenga fedha za kilometra tatu na bajeti ya 2014/2015 wametenga fedha za kutengeneza barabara urefu wa kilometra mbili, ina maana kwa utaratibu huu barabara hii itatengenezwa kwa miaka takribani name. Je, Serikali haioni kwamba azma ya Mheshimiwa Rais haikuwa hiyo, wanaenda kinyume kabisa na azma hiyo? Ni lini watatenga fedha za kutosha kuhakikisha kwamba barabara hiyo inaisha kwa wakati? (Makofii)

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, kwa kuwa kikao cha RCC cha Mkoa kilipitisha barabara tano kupandishwa daraja kuwa barabara za mkoa na Kamati ilitembelea barabara hizo lakini mpaka sasa hivi Serikali haijatoa majibu yoyote ya kupandisha daraja barabara hizo ambazo ni barabara ya Singida – Kinyeto – Sagara; barabara ya Chikuyu – Chibumagwa – Mpangani – Ikasi; barabara ya Sekenke – Tulia – Kidaru; barabara ya Mungaa – Tuntu – Mang’onyi na barabara ya tano ni Singida – Mtamaa – Minyoge – Mtavira – Mkenene na

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Iyumbu. Je, ni lini Serikali itarudisha majibu barabara hizi kupandishwa daraja ambapo mpaka sasa hivi zina hali mbaya ambapo kwa ngazi ya halmashauri hazina fedha za kuzihudumia?

**SPIKA:** Hapo umeongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Chilolo kwa namna anavyofuatilia matengenezo na ahadi za Rais katika barabara hii, mara kwa mara amekuwa ananiulizia itatekelezwa lini. Majibu ni kwamba tayari ahadi ya Rais kama nilivyosema kwenye jibu la msingi tumeshaanza kuitekeleza na tunasema tunatekeleza ahadi hii kwa awamu kutokana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, nafikiri nikumbushe kwamba tulisema sera yetu ya kujenga barabara za lami tutaanza kwanza na barabara kuu zile zinazounganisha makao makuu ya mikoa na mikoa. Tutakapomaliza, nguvu kubwa tutaipeleka kwenye barabara za mikoa. Kwa hiyo, sasa hivi tunapelekea nguvu kubwa kwenye barabara kuu zinazounganisha mikoa na mikoa. Kwa sababu ya umuhimu wa barabara hii ndiyo maana kila mwaka tunaweka fedha, kwa mfano, kwa mwaka huu wa 2015/2016, Mkoa wa Singida umeshatenga shilingi bilioni 1.41 kwa ajili ya matengenezo na kuendelea kujenga barabara hii. Kwa hiyo, tayari kuna *commitment* ya Serikali katika kutekeleza ahadi hii ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, swalı lake la pili kuhusu barabara ambazo ziliwasilishwa kwa ajili ya kupandishwa hadhi baada ya RCC kuitisha, huo ni utaratibu tu wa kisheria. Ille Kamati bado inaendelea kuchambua, watakapokamilisha tutatoa taarifa ni barabara zipi zimeweza kupita na barabara zipi zitaendelea kuhudumiwa na halmashauri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Paresso swalı la nyongeza!

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swalı dogo la nyongeza. Kwa kuwa swalı la msingi linazungumzia kuhusu ahadi za Rais na ahadi hiyo pia ilitolewa katika barabara ya Karatu – Njiapanda - Mang'ola – Lalago. Kwa jinsi ambavyo Waziri amejibu hapo amesema msisitizo unatolewa kwa barabara zinazounganisha mikoa na mikoa na barabara hii ya ahadi inaunganisha mkoa wa Arusha na Simiyu. Je, ni lini sasa barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Karatu - Lalago ni kweli ni barabara inayohudumiwa na Wizara ya Ujenzi lakini ni barabara ambayo haipo kwenye mpango kwa sasa wa kuanza kujenga kwa kiwango cha lami. Tulitoa taarifa, kuna kitabu ambacho kinaonyesha miradi ya barabara zile ambazo zimekamilika katika Awamu hii ya Nne na zipo ambazo zinaendelea. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge tukae tuweze kuchambua tuone barabara hiyo iko katika hatua ipi kwa sababu zipo barabara ambazo zipo kwenye usanifu uliokamilika na ziko barabara ambazo usanifu unaendelea. Kwa hiyo, naona nitakaa naye ili kusudi niweze kuona barabara hiyo iko katika hatua gani ya ujenzi.

**SPIKA:** Ni kweli swalii kama jipya inakuwa siyo rahisi kupata majibu. Sasa ni Wizara ya Kazi na Ajira, Mheshimiwa Betty Machangu anauliza swalii hilo.

Na. 176

**Ukosefu wa Ajira kwa Vijana Wanaohitimu  
Vyuo vya Elimu ya Juu Nchini.**

**MHE. BETTY E. MACHANGU** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikisema mara kwa mara kwamba vijana wanaosoma katika vyuo vya elimu ya juu wajiajiri baada ya masomo yao:-

Je, Serikali inaweza kuueleza umma wa Watanzania kuwa ni kwa namna gani kijana huyu anayetoka chuoni baada ya kumaliza masomo yake anaweza kujiajiri bila mtaji, hasa ikizingatiwa kuwa Serikali imeshindwa hata kumsaidia Mtanzania wa kipato cha chini kukopa kwenye benki kwa sababu ya riba kubwa ya asilimia 18 hadi asilimia 24?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kazi na Ajira, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua changamoto za ukosefu wa ajira kwa vijana wanaohitimu vyuo vya elimu ya juu pamoja na vijana wote kwa ujumla. Kwa kutambua hilo, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya kuwawezesha vijana kushiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo ya nchi yetu kwa njia ya kujiajiri pamoja na kutengeneza fursa za ajira kwa wengine. Baadhi ya mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Utekelezaji wa programu ya ajira kwa vijana ya mwaka 2014/2015 hadi 2016/2017. Programu hii imewalenga vijana kuanzia umri wa miaka 15 - 35 kwa kuwekea vijana mazingira wezeshi ya kujajiri na kuajiri wengine hasa kwa kuzingatia maeneo matatu ya matokeo ambayo ni kuwajengea uwezo kwa njia ya mafunzo ya stadi za ujasiriamali, stadi za maisha na stadi za kazi ili waweze kuhimili ushindani katika soko la ajira; kuwapatia mitaji ambayo ni mikopo yenyе masharti nafuu bila hitaji la dhamana ili vijana waweze kujajiri kwa kuanzisha ama kuendeleza shughuli za kiuchumi kwa manufaa yao na nchi kwa ujumla wake; na mwisho ni kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli ya uzalishaji na biashara kwa vijana ambapo halmashauri zote zimeelekezwa kutenga maeneo hayo na agizo hilo mpaka sasa limetekelizwa kwa asilimia kubwa. Utekelezaji wa programu ya ajira kwa vijana unatarajia kuzalisha ajira 840,000 kwa kipindi cha miaka mitatu.

(ii) Utekelezaji wa Mpango wa kukuza ajira zenyе staha kwa vijana vijiji unaojulikana kama uvezeshaji wa vijana kuwekeza katika kilimo kwa kuanzisha vilabu vya vijana vya kilimo vijiji. Mradi huu ni wa miaka mitano na umegawanywa katika awamu mbili ambapo awamu ya kwanza inaitwa production phase. Vijana wataunganishwa na taasisi za fedha, kupitia Mfuko wa Dhamana wa Kilimo wa Vijana utakaowawezesha kupata mikopo yenyе masharti nafuu kwa mfumo wa kilimo cha mkataba yaani *contract farming*.

Awamu ya pili ya mradi inalenga katika mnyonyoro wa thamani wa mazao ya kilimo ambapo vijana watawezesha kuchakata mazao ya kilimo na kuyauza kama bidhaa. Mradi huu unahusisha mikoa yote 25, Tanzania Bara ambapo kila mkoa utahusisha wilaya mbili na kila wilaya itatoa vijana 150. Kila wilaya itatoa vijiji vitano na kila kijiji kitatoa vijana 30.

Mheshimiwa Spika, mipango hii yote inalenga kutumia ipasavyo nguvu kazi ya vijana katika kuliletea Taifa maendeleo na kupunguza kiwango cha ukosefu wa ajira nchini. Kinachokwamisha utekelezaji wa mikakati hii ni ufinyu wa bajeti. Mathalani programu ya ajira kwa vijana ambapo pamoja na Bunge kuidhinisha bajeti ya shilingi bilioni tatu kwa ajili ya utekelezaji wake hadi sasa fedha hajijapatikana ili tuanze utekelezaji.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Betty Machangu swali la nyongeza!

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru naomba niulize maswali ya nyongeza mawili.

Mheshimiwa Spika, hii mipango ilivyoelekezwa na Serikali inaonekana ni mipango isiyoendelevu maana yake ni kwamba ina muda maalum lakini idadi ya vijana inaendelea kuongezeka. Katika sensa ya mwaka 2012, tafiti zinaonyesha kwamba asilimia 63 ya Watanzania ni kundi la wategemezi.

Je, ni lini Serikali itaweka mipango ya kudumu ya kuajiri vijana au mipango ya kudumu ya kuendelea kuwawezesha kujajiri? (Makofij)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, iko mikoa ambayo ina ardhi kidogo kwa mfano Kilimanjaro na upo mpango ulianzishwa na Mwalimu Nyerere na nadhani ukaendelezwa na Mheshimiwa Mkapa wa kuondoa vijana kwenye maeneo yale ambayo hakuna ardhi na kuwapeleka katika mikoa mingine Tanzania ambayo kuna maeneo ya kulima ya kutosha. Je, Serikali ina taratibu gani ya kuendeleza mpango ule?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, mpango huu pamoja na kwamba tumesema ni wa miaka mitatu lakini ni endelevu kwa maana kwamba ni miaka mitatu mitatu. Baada ya miaka mitatu kuisha mpango huu unaendelea tena kwa utaratibu huohuo wa miaka mitatu kila wakati. Kwa hiyo, ni endelevu si kwamba baada ya miaka mitatu basi tutakuwa tumekomea hapo. Ndiyo maana hata mipango ya maendeleo ya nchi tunafanya kwa miaka mitano, mitano haina maana kwamba tukifika miaka mitano tena hatutaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hili la pili, namshukuru sana na nampongeza katika hili analolizungumzia lakini hata huu mpango wa pili ambao niliuzungumzia unalenga hilohilo la kuhakikisha kwamba vijana wanaingia kwenye maeneo ya uzalishaji vijiji ambayo yanaweza yakawa mazuri kwa kilimo, wanatengewa maeneo ya kilimo na wanaendesha utaratibu huo wa kilimo ili waweze kujajiri katika kilio. Nimeueleza vizuri sana katika sehemu ya pili ya jibu langu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Engineer Masauni.

**MHE. ENG. HAMAD YUSSUF MASAUNI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa fursa hii. Naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wa Jimbo la Kikwajuni ni mfano mzuri wa jamii ambayo imejikusanya pamoja na kuendeleza mfumo wa kibenki ambao umekuwa na tija sana kwa wajasiriamali kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu na ambayo haina riba. Je, ni fursa gani ambazo zipo Serikalini za kuwasaidia wananchi hao kukabiliana na changamoto hizi ikiwemo za uhaba wa mitaji pamoja na mafunzo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI NA AJIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa kuanzisha utaratibu huo wa kuwa kwenye vikundi. Kama ambavyo tumekuwa tukisema kila wakati, Serikali itasaidia zaidi vijana au watu ambao wamekaa kwenye vikundi na kuanzisha miradi fulani, wameanza kujiweka labda mitaji na Serikali iweze sasa kuongezea ile mitaji na mambo mengine kama elimu ya ujasiriamali. Kwa hiyo, nina hakika katika utaratibu huu kama akiwasiliana na Serikali kama ni ya Mapinduzi au vyovyyote vile hate Serikali ya Jamhuri ya Muungano wanaweza wakasaidiwa kwa sababu wameweka mwanzo mzuri.

**SPIKA:** Ahsante. Twende swali la mwisho la Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Dkt. Henry Shekifu atauliza.

Na. 177

### **Kilimo cha Kutumia Utaalamu wa GMO**

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU** aliuliza:-

Kilimo cha mazao kwa kutumia utaalam wa GMO kimeshika kasi katika nchi za Afrika hasa Afrika Kusini, Burkina Faso na kadhalika:-

(a) Je, Tanzania ina mpango gani wa kuanzisha kilimo hicho kinachoonyesha kuongeza uzalishaji mara dufu katika mazao ya pamba na kadhalika?

(b) Je, wataalam wetu wamejifunza utaalam huo na wanatoa ushauri gani kwa aina hii ya kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO (K.n.y WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Henry Daffa Shekifu, Mbunge wa Jimbo la Lushoto, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa matumizi ya sayansi katika maendeleo ya kilimo nchini hasa kutokana na athari za mabadiliko ya tabia nchi yanayosababisha ukame, mafuriko, mtawanyiko mbaya wa mvua pamoja na kuibuka kwa magonjwa na visumbufu vipyta vya mimea na hivyo kuathiri uzalishaji wa mazao.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia changamoto hizi, Serikali imeandaa mpango kabambe wa kuendeleza mazao ya pamba, muhogo, mahindi na migomba kwa kutumia utaalam wa uhandisi jeni. Chini ya mpango huo, Serikali imeimarisha uwezo wa watafiti, miundombinu, maabara na mashamba maalum kwa ajili ya kufanya utafiti unaolenga kutatua changamoto hizo. Hata hivyo, utekelezaji wa mipango hiyo umeathiriwa na uwepo wa kipengele cha dhima kali (*strict liability*) katika Kanuni za Kusimamia Matumizi Salama ya Bioteknolojia (*The Environment Management Biosafety Regulations*) za mwaka 2009 ambacho kinalenga kuwajibisha watafiti wa mazao ya GMO endapo madhara yoyote yatatokea hata kama hawakukusudia kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa manufaa makubwa ya teknolojia ya uhandisi jeni katika kuleta mapinduzi ya kilimo, Serikali imefanya marekebisho ya Kanuni hizo kwa kuondoa dhima kali (*strict liability*) katika utafiti na hivyo kuwezesha utafiti katika mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, wataalam wetu wamejifunza utaalam huo na wanao uwezo wa kuitumia teknolojia hiyo ambayo katika utafiti wa maabara kwa kutumia uhandisi jeni wameweza kugundua jeni (*genes*) katika muhogo ambazo zina ukinzani wa magonjwa ya batobato na michirizi kahawia ya muhogo. Kwa sasa watafiti hao wanaendelea na utafiti huo katika ngazi za mashamba maalum ili kuwawezesha kugundua aina za muhogo ambazo zina ukinzani dhidi ya magonjwa hayo. Kwa kuzingatia manufaa ya uhandisi jeni katika kilimo, wataalam wamekuwa wakishauri matumizi ya teknolojia hiyo kama matokeo ya utafiti yataonyesha kuwa matumizi ya mazao ya GMO ni salama na hayana madhara yoyote kwa afya za binadamu, wanyama na mazingira. Aidha, Serikali itaendelea kuwaelimisha na kukuza uelewa kwa wakulima na wananchi kwa ujumla kuhusu manufaa ya teknolojia ya uhandisi jeni katika maendeleo ya kilimo.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Shekifu swali la nyongeza.

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuipongeza Serikali kwa kuondoa kifungu cha dhima kali kwa sababu kifungu hiki ndiyo kilikuwa kinawakatisha tamaa sana wataalam wetu nia ya kuendeleza utaalam huu. Serikali inachukua hatua gani baada ya kuondoa kifungu hiki kutangaza ratiba inayoleweka ya kuweza kuingia katika utaalam huu wa kilimo hiki? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa yako mazao ambayo utafiti wake hauna matatizo na iko dhana ya wasiwasu ya kwamba kilimo hiki kinaweza kuleta madhara katika afya za watu. Kwa nini tusiendelee na utafiti uliofanyika katika mazao ya biashara kama pamba ili tuzalishe tuongeze uzalishaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa zamani wa Kilimo na Chakula na Ushirika

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. ADAM K. MALIMA (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kwanza nianze kupongeza majibu mazuri ya Mheshimiwa Pindi Chana kwa niaba ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kile kipengele cha dhima kali kilikuwa kinatukwaza, kilikuwa kwenye Sheria ya Mazingira, Waziri Mahenge na wenzake wamekifanya kazi na tumekubaliana kwamba kiondoke. Hata hivyo, siyo kwamba kimeondoka kwa sababu hatuweki tahadhari, kilichofanywa ni kwamba ile *strict liability* imeondoka lakini tumeweka mkakati kwamba kila zao linalofanyiwa utafiti litapata kama miaka mitatu ya kufanyiwa utafiti na kuangalia madhara yake.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Shekifu, mazao yale ambayo yanalengwa, pamba, migomba kuondoa matatizo yale ya mnyauko, mihogo kuondoa batobato na kadhalika, yanafanyiwa utafiti Kenya, Uganda, wenzetu wameshakuwa zaidi ya miaka mitatu, minne mbele kwa maana ya research yearsterms. Kwa hiyo, sisi ambao ndiyo wazalishaji wakubwa wa chakula kusema kweli katika Kanda yetu hii tumekuwa nyuma kwa sababu ya kipengele hiki. Matarajio ni kwamba kipengele hiki kimefunguliwa na kwamba wakulima wetu watapata nafasi ya kutumia ujuzi mkubwa wa wataalam wetu.

Mheshimiwa Spika, hili la pili la upeo wa wataalam wetu, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba, nilipata nafasi ya kwenda Des Moines Marekani kwenye Mkutano Mkuu wa Watafiti wa Kilimo Duniani na wataalam wa Tanzania mmojawapo akiwa Dkt. Roshan Abdallah, mama mmoja yuko pale, wenzetu wanagombea kuwapa mikono wataalam wetu kwa sababu ya uwezo wao mkubwa sana katika utafiti wa mihogo na migomba na kadhalika lakini sisi wenyewe tunawapiga nyundo. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niwahakikishie tu Wabunge kwamba upande wa base ya wataalam, tuna wataalam wakubwa sana kwenye masuala ya uhandisi jeni, wako hapa Mikocheni na wako kwenye Kituo cha WEMA hapa Makutupora. Naomba niwasihii Waheshimiwa Wabunge ambao watapata nafasi na Mheshimiwa Dkt. Msolla anawajua, waende wakaangalie mafanikio makubwa ya utafiti ambao ni wa kwetu wenyewe, kwa sababu ya sheria ambazo tumejiwekea, wanakwenda Uganda na Kenya kuwapa msaada wenzetu bila kutusaidia sisi wenyewe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Haroub.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mimi kwa taarifa ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao tunasimamia Wizara hii ya Sayansi, Mawasiliano na Teknolojia. Juzi tu Jumamosi tulipata nafasi ya kwenda kutembelea Kituo cha Utafiti cha Makutopora ambacho kakitaja Mheshimiwa Naibu Waziri sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha ni kwamba pamoja na umahiri na umakini walionao wataalam wetu lakini Serikali inawaangusha kwa sababu hata maabara iliyopo hapo Makutupora ni jengo tu halina vifaa na utafiti au research ni vifaa vya kisasa. Pamoja na kwamba tunao watafiti mahiri na makini lakini Serikali haiwapi vifaa vya kufanya utafiti, je, utafiti huo utafanyika kwa mikono na mdomo tu? (Makofij)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. ADAM K. MALIMA (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):** Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Haroub kwa *ku-point out* hilo suala la matatizo ya WEMA kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na pia kwa suala la sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililokuwepo, kwa sababu ya kile kipengele cha *strict liability*, tulikuwa tumewazuia wale hata kufanya utafiti katika maeneo yale pale. Matokeo yake vile vituo vya WEMA viko vitano Kanda ya Afrika kwa maana ya Kenya, Tanzania, Uganda, Malawi na SouthAfrica. Kituo cha Tanzania ambacho ndiyo kilikuwa *targeted* kwa sababu ya uzalishaji wetu mkubwa kimebaki nyuma. Wenzetu wa Kenya na Uganda wamefikia hatua kubwa ya utafiti wa mahindi wakati sisi ndiyo walimaji wakubwa. Ndiyo maana tukasema kwa kuondoa kipengele kile, matarajio yetu ni kwamba wanasyansi wetu tumewafungua, tumewapa nafasi, kwenye bajeti ya Serikali ya mwaka huu, kuna kipengele maalum cha *retention* ambapo pesa za ziada zinakwenda kwa ajili ya watafiti na COSTECH ili kuwekeza hela kwa ajili ya utafiti huo ambao unalenga ku-guarantee usalama wa chakula na usalama wa lishe ya Watanzania.

**SPIKA:** Ahsante. Maswali yamekwisha, naomba nitambue baadhi ya wageni tulionao.

Wageni wa Mheshimiwa Kebwe Stephen Kebwe, Naibu Waziri wa Afya na Usatawi wa Jamii ambao ni wanafunzi 58 kutoka Sebastian Kolowa Memorial University (SEKOMU) Lushoto. Naomba msimame pale mlipo, ahsanteni sana. (Makofij)

Pamoja nao yupo Ndugu Ernei Joseph mwanafunzi ambaye pia ni mlemavu yuko katika Chuo Kikuu cha Dodoma, ameambatana na wenzake watatu. Ahsante tulikuona. Mtakapotoka tumewasogezea kiti ambapo mniamweka ndugu yenu pale anakwenda kwenye mashine inayohusika itamshusha ataingia kwenye gari lake, msimbebe kama mlivyomleta hapa, kidogo ilikuwa siyo vizuri. Karibu sana Ndugu Joseph kuweza kupata nafasi kuona shughuli za Bunge. (Makofi)

Tuna wageni saba wa Mheshimiwa Mary Nagu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine, Morogoro, wakiongozwa na Ndugu George Magway, inawezekana wako basement tuna tatizo la ukumbi.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Innocent Lwabushaija ambao ni wanafunzi 60 wa vyuo vikuu mbalimbali nchini wazaliwa wa Wilaya ya Kyerwa, Kagera. Naomba hawa wote wasimame kama wamo ndani humu. Ahsante, karibuni sana, kikubwa ni kusoma kwa bidii. (Makofi)

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale ambaye ni Ndugu Fadhili Mzumbwe, mwanafunzi wa St. Aggrey Mbeya. Huyu mwanafunzi naye asimame, nadhani mtu mmoja atapata nafasi, ahsante sana. (Makofi)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Joshua Nassari ambao ni Ndugu Meyasi Mollel, Mkurugenzi wa Serengeti Preservation Foundation na Ndugu Humphrey Pallangyo, Mjumbe wa Bodi ya Serengeti Preservation Foundation. Naomba hawa wasimame kama wapo ndani, ahsante, karibuni sana. (Makofi)

Tuna wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo, tuna wanafunzi 80 na walimu nane wa Shule ya Montesori Kiloleni Mwanza. Naomba hao wote kama wapo ndani wasimame. Ahsanteni sana na karibuni sana. (Makofi)

Tuna wanafunzi 65 wa shule ya msingi Nala, Dodoma. Naomba nao wasimame kama wapo ndani, ahsante sana na karibuni. (Makofi)

Tuna wanafunzi 47 na walimu sita kutoka shule ya msingi *Southern Highlands* iliyopo Mafinga Iringa na wenyewe wasimame kama wamo ndani. Ndiyo ninyi leo mmekaribishwa kwa *Speakers Platform?* Maana yake leo mmekuwa VIP kwelikweli! (Kicheko/Makofi)

Tuna wajumbe 10 pamoja na watoto 20 kutoka Asasi ya Shiriki Malezi Endelevu (SHIME). Naomba hawa wasimame kama wamepata nafasi.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Halafu tuna wanafunzi 57 na walimu 5 kutoka shule ya msingi ya St. Theresia ya Mbezi Louis. Kama wamepata nafasi wanakaribishwa wasimame tuwaone. Ahsanteni sana, mmetoka mbali karibuni sana, watoto msome vizuri. (Makofii)

Napenda kuwaambia wananchi na taasisi mbalimbali wanaotaka kuja Bungeni wasisubiri zile siku za mwisho, nafasi humu ndani inakuwa hakuna kabisa. Nashauri wawe wanaomba toka tunapoanza ili kusudi waweze kupangiwa nafasi.

Nimeombwa nitangaze, sasa huyu Mbilinyi F.A. sijui kama ndiyo Mbilinyi wangu yule au mwingine, anawatangazia Wabunge na watumishi wa madhehebu ya kiprotestanti kwamba leo Jumanne tarehe 9 kutakuwa na ibada ukumbi wa Msekwa, ghorofa ya pili, Kanisani, saa nane mchana. Sijui kama lazima iwe saa nane mchana au vinginevyo lakini tangazo ndivyo linavyosema.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mnajiona ninyi mko sawa? Haya sasa tunaanza, Mheshimiwa Martha.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nitumie Kanuni ya 47(1), kwa idhini yako ama nisome au niseme hoja yangu.

**SPIKA:** Endelea.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, kumetokea jambo ambalo si zuri sana katika mkoa wangu wa Singida hususan katika Wilaya ya Ikungi kwenye eneo la Mang'onyi ambako kuna Mgodi wa Madini wa Ashanti. Hivi sasa navyoongea vijana takribani 2,000 wameshindwa hata kutoka ndani ya nyumba zao ama wengine wako kwenye maeneo ya migodi wamejificha kwa sababu wana hofu ya kupigwa mabomu na askari.

Mheshimiwa Spika, Ashanti walipewa kibali cha kufanya utafiti katika eneo lile takribani kwa miaka nane, walipomaliza kibali kile wakapewa leseni ya kuchimba, wakati wote ule wananchi walikuwa wanaendelea na shughuli zao kwenye maeneo yale. Alipopewa leseni alitakiwa awalipe fidia wananchi wale lakini mpaka sasa ni miaka mitatu hajalipa fidia na wananchi bado wako pale.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Kwa hiyo, vijana ambao wanaishi kwenye maeneo yale wameamua kuendelea na shughuli zile ambazo walikuwa wakifanya kujitafutia riziki.

Mheshimiwa Spika, askari wameenda na imekuwa ni mazoea vijana wanateseka na mimi ni Mbunge wa eneo lile nimeshindwa kuvumilia, naomba leo Serikali jambo hili ijadiliwe ama Serikali iingilie kati na itoe majibu. Ikiwezekana Waziri wa Nishati na Madini siyo Naibu Waziri aende mwenyewe akakutane na wale vijana 2000 wanaoteseka na familia zao, wake zao wanateseka, watoto wanateseka kwa sababu ya mtu aliyepata leseni hafanyi kazi halafu anawazuia watu na kulipa fidia halipi. Naomba sana tujadili ama Serikali iingilie kati.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kuhusiana na jambo hili, siwezi kukubali mimi ni Mbunge wa eneo hilo.

**SPIKA:** Hakuna hoja, ulikubaliwa? Un gesoma ile Kanuni inakuambia utapewa dakika tano, ikishajieleza inakuwa juu ya Spika kuona umuhimu wa hoja hiyo. Sasa nasema tumekusikia, umesema kwa nguvu wala sisi hatujui hoja hiyo na utapata maelezo kutoka kwa wanakaohusika. Sasa namuita Mheshimiwa Silinde.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** No, no, Mheshimiwa Waziri kuhusu hili naomba mlifanyie kazi kwa sababu sisi wengine ndiyo tumelisikia sasa hivi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri sijakuita.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Spika, tumekwishalifanyia kazi nilitaka kutoa taarifa.

**SPIKA:** Sijakuita sasa naomba ukae. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako kupitia Kanuni hii ya 46 inayohusu maswali kujibiwa kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kipindi cha maswali, swali langu namba 171 ambalo lilikuwa linahusu mambo ya mawasiliano, Waziri majibu yake ya awali yalikuwa ni sahihi lakini kuna swali dogo la nyongeza ambalo nimeuliza ndani ya Bunge lako Tukufu hapa juu ya wizi ambapo wananchi wanakatishwa data wakati hawatumii hizo data katika maeneo ya vijijini.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri aliyejikuwa anajibu hapa amekiri kwamba yeye halifahamu kwa sababu hiyo Wizara siyo yake, hiyo natoa excuse, nimepata majibu ya nyongeza kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali lakini yake yalikuwa yanahu zaidi masuala ya electronic pamoja na cybercrimes.

Mheshimiwa Spika, swali langu kubwa nililokuwa nauliza na ambalo ndiyo imekuwa kero kwa wananchi ni kwamba wanaponunua vifurushi, kwa mfano unaponunua kifurushi cha Sh.1000 unapewa na data na mtu mwenyewe unatumia labda simu kama Nokia ya tochi data ile hutumii. Huu unaitwa ni wizi wa waziwazi ambao unafanywa na makampuni ya simu. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, swali langu halijajibiwa vizuri. Naomba Mwongozo wako kwamba uitake Serikali ilete majibu sahihi ndani ya Bunge ili wizi huu usiendelee kama watu wanapewa data, kama mtu anapewa mawasiliano yake apewe kwa sababu wizi huu umekuwa ni mkubwa, watu wamekuwa wakikatwa pesa zao hususan wananchi wa vijijini. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Mwongozo wako juu ya suala hilo. Ahsante. (Makofii)

**SPIKA:** Hili swali limejibiwa vizuri sana kwa sababu Waziri amesema, mimi sifahamu nitapeleka kwa wanaohusika, angesema nini? Haya Mheshimiwa Paresto!

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba Mwongozo wako kwa Kanuni ya 47 kuhusu jambo la dharura.

Mheshimiwa Spika, kuitia vyombo vyaa habari jana na juzi tumeona wanafunzi wa Vuo Vikuu vyaa Kampala University na St. Joseph Arusha wamekuwa kwenye mgomo wa takribani siku ya tano kwa Chuo Kikuu cha Arusha cha St. Joseph na Kampala University ni siku ya pili leo wako kwenye mgomo wakilalamikia mambo kadha wa kadha likiwemo suala la mitaala lakini pia suala la miundombinu hafifu. Wanafunzi wa Kampala University wanachogoma na malalamiko yao makubwa ni kwamba Kitivo cha Afya, wanafunzi wa famasia na medicine wakimaliza vyuo hawapati ajira kwa sababu hakuna usajili uliofanyika, chuo hakijasajiliwa. (Makofii)

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wako kwenye mitihani lakini wamegoma. Mitihani haiendelei, wako ambao wamefukuzwa chuo lakini Serikali inatumia nguvu kubwa, tumeona jana kuitia vyombo vyaa habari wanafunzi wanafukuzwa na maji ya washawasha, wanapigwa mabomu badala ya kushughulikia tatizo hilo.

## **NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Spika, niseme mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii, tarehe 27 Mei, Serikali ilituletea taarifa kwamba itachukua hatua, lakini mpaka leo ni wiki ya pili, hakuna hatua za uhakika zilizochokuliwa ili kunusuru hali inayoendelea katika vyuo hivi. Kwa hiyo, naomba suala hili tulijadili tuone namna gani tunaondoa haya matatizo kwa sababu kama Kamati na Serikali hatujapata majibu na hakuna kilichofanyika. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Kumbe unafahamu kwamba Kamati ipo, mimi ninachotaka wamalize upesi tupewe taarifa. Ninyi siyo executive. Mheshimiwa Bulaya!

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako au ikiwezekana kuitaka Serikali kuzungumzia swali la Mheshimiwa Sanya kuhusu vipodozi.

Mheshimiwa Spika, vipodozi ambavyo vimezungumziwa ni vipodozi tu vya kujipamba lakini kuna tatizo kubwa sasa hivi limeingia kwa watu kuweka makalio bandia na manyonyo bandia. Tatizo hili ni kubwa na kuna picha zinasambaa katika mitandao athari yake watu wanapata kansa na hata kuharibika miili yao na kutoka majeraha makubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hapa Tanzania jambo hili limeingia na ni hatari kubwa sana, mabinti wanaharibika maungo yao na wanapata magonjwa ya kansa. Sasa Serikali isiangalie suala tu la vipodozi la mikorogo usoni, jambo hili la watu kuweka makalio na matiti bandia limeingia na linaleta madhara makubwa sana hasa ikiwepo kansa. Kwa hiyo, Serikali ingezungumzia kwa kina jambo hili.

**SPIKA:** Nakushukuru kwa taarifa. Waheshimiwa Wabunge, tunaahirisha shughuli mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 4.33 Asubuhi Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatano,  
Tarehe 10 Juni, 2015, Saa Tatu Asubuhi)*